# JARIDA la Mamlaka ya Serikali Mtandao

eGA ISO 9001: 2015

Toleo la 7 | Januari - Machi 2024



**"VIONGOZI TUMIENI MFUMO WA e-MREJESHO KUPOKEA MAONI YA WANANCHI."**

**Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Yaliyomo

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu....1
Rais Dkt. Samia awataka Viongozi kutumia Mfumo wa e-Mrejesho ....2
e-GA yapata Ithibati ya ubora Kimataifa....3
Kamati ya PAC yaipongeza e-GA kwa ubunifu....4
Tutahakikisha matumizi ya TEHAMA Serikalini yanazidi kuimarika: SIMBACHAWENE....5
Wanawake wahimizwa kutumia TEHAMA kukuza uchumi....6
Wekeni Mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Serikali Mtandao: KIKWETE ....7
Ushirikiano wa e-GA na e-GAZ wachochea mageuzi ya kidijitali Visiwani Zanzibar....8
Ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu wachangia uboreshaji wa huduma jumuishi....9
e-GA endeleeni kufanya kazi kwa bidii na uadilifu: SIMBACHAWENE ....10
Wataalamu wa TEHAMA serikalini wapewa mafunzo ....11
Watumishi wa e-GA watakiwa kujiepusha na rushwa ....12
Ongezeko la magonjwa sugu yasiyoambukiza tishio kwa watumishi ....13
Tengeni muda wa maisha binafsi kuepuka ugonjwa wa afya ya akili: Dkt KWEKA....14
Miaka 3 ya Rais Dkt. Samia: Serikali Mtandao yazidi kuimarika ....15
Kutoka kituo cha utafiti na ubunifu - eGOVRIDC ....17
Matukio katika picha ....18

# Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu



Karibu katika toleo la saba la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma bora kwa Umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utaweza kufahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema.



**Mhandisi Benedict B. Ndomba**
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**



> "Nendeni mkatumie mfumo wa e-Mrejesho nyie mpate mrejesho na sisi tupokee mrejesho lakini na wananchi wapate taarifa kupitia huu mfumo na ndivyo tutakavyoweza kufanya kazi kwa haraka na kwa ufanisi zaidi tukitumia mifumo"
>
> Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan
> Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# RAIS DKT. SAMIA AWATAKA VIONGOZI WA UMMA KUTUMIA MFUMO WA e-MREJESHO KUPOKEA MAONI YA WANANCHI

**Ikulu - Dar Es Salaam**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan, amewataka viongozi wa umma kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Mawasiliano wa e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu Serikali na pia kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo.

Dkt. Samia ametoa maelekezo hayo Machi 13 mwaka huu Ikulu jijini Dar es Salaam, mara baada ya kuwaapisha viongozi aliowateua katika nafasi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Alisema kuwa, viongozi wa umma wanapaswa kufahamu na kutumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA iliyopo Serikalini katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kutumia Mfumo wa e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi na kutoa mrejesho kwa wananchi pamoja na Serikali juu ya utekelezaji wa maoni hayo.

Alibainisha kuwa, viongozi wa umma wanapaswa kuitumia vizuri mifumo mbalimbali ya kielektroniki inayopelekwa Serikalini, ili isaidie kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wao na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa wakati mahali walipo.

Akizungumza kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA Serikalini, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba amesema kuwa, e-GA itaendelea kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha yanaleta tija kwa kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi kwa wakati mahali walipo.

Vilevile, Mfumo huu unasaidia kuokoa muda na fedha kwani mwananchi halazimiki tena kusafiri umbali mrefu kwenda katika ofisi ya umma kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko yake au kufuatilia utekelezaji wake na badala yake anaweza kufanya hivyo kidijitali kupitia simu yake ya kiganjani mahali alipo, alisema Ndomba.

"Zamani ilikuwa mtu akihitaji kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma inayotolewa na taasisi ya umma ilimlazimu kufika katika taasisi hiyo na kuwasilisha malalamiko yake kwenye sanduku la maoni au kuwasilisha barua katika taasisi hiyo na kisha kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wake, lakini kwa sasa anaweza kuwasilisha maoni hayo kidijitali", alifafanua Ndomba.

Alieleza kuwa, mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kisha kuchagua namba 9 na kisha namba 2, njia zingine ni kupitia simu janja kwa kupakua Aplikesheni (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye Play Store na Apple Apps Store, na kwa njia ya Tovuti ya emrejesho.gov.go.tz.

Aliongeza kuwa, ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha lalamiko lake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu lalamiko hilo kuhamishwa kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine na pia unamruhusu mwananchi kukata rufaa kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu lalamiko lake.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwani lalamiko linapofika kwenye taasisi litaonekana kwenye ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila Afisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana, pia mfumo unafanya uchambuzi wa taarifa na kumuwezesha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais UTUMISHI na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyowazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia Dashboard maalum", alisema Ndomba.

Katika kuhakikisha mifumo ya TEHAMA Serikalini inawasiliana na kubadilisha taarifa Ndomba alibainisha kuwa, mfumo wa e-Mrejesho unao uwezo wa kubadilishana taarifa na mifumo mingine kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini 'Government Enterprise Service Bus-GovESB' na tayari mifumo mbalimbali imeunganishwa na e-Mrejesho kupitia Mfumo wa GovESB.

Mfumo wa e-Mrejesho umetengezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi zote za Umma zimeunganishwa.

# e-GA YAPATA ITHIBATI YA UBORA KIMATAIFA

## ISO 9001: 2015 CERTIFIED



Kaimu Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi na Ubora wa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Farida Juma

"Lengo letu ni kuendelea kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma ili kuboresha utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma za Serikali kidijitali na hivyo kupunguza muda wa kutoa huduma na kuongeza ufanisi"

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imethibitishwa kuwa Taasisi inayofuata viwango vya ubora Kimataifa (ISO) katika kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma kulingana na Kiwango cha Ubora wa Kimataifa (ISO 9001:2015).

Hayo yamebainishwa na Kaimu Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi na Ubora wa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Farida Juma, alipofanya mahojiano maalum na mwandishi wetu Machi 20 mwaka huu ofisini kwake jijini Dodoma.

"Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), tumepokea cheti cha uthibitisho wa kiwango cha ubora wa kimataifa na sasa tunatambulika kimataifa kama Taasisi inayofuata viwango vya ubora wa kimataifa katika kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma na mifumo salama ya kieletroni kwa Taasisi za Umma", alisema Farida.

Aliongeza kuwa, katika ripoti ya mwaka 2022 ya utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (WB) kuhusu Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani katika utoaji wa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi (GovTech Maturity Index), Tanzania ilitajwa kushika nafasi ya pili barani Afrika na nafasi ya kwanza Afrika Mashariki,hii inadhihirisha namna ambayo e-GA imejipanga kutoa huduma bora kwa viwango vya kimataifa.

Alisema kuwa, kupata uthibitisho huo wa ISO 9001:2015 kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ni hatua muhimu katika kuonyesha msimamo wa Mamlaka wa kutoa huduma bora zaidi za TEHAMA kwa Taasisi za Umma na kuboresha utendaji kazi.

Aidha, alibainisha kuwa mchakato wa kupata cheti hicho ulianza kwa watumishi wa e-GA kupatiwa mafunzo na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ili kuwawezesha watumishi hao kukidhi vigezo vya utoaji huduma kwa wateja wake kulingana na matakwa ya kiwango cha ubora.

Aliongeza kuwa, e-GA imejizatiti kutoa mifumo bora na salama ya kieletroniki kwa Taasisi za Umma na kuendelea kuboresha huduma zake ili kukidhi mahitaji ya kisheria, viwango vya kimataifa na matarajio ya wateja wake.

"Tutahakikisha ufanisi unaongezeka katika kutoa huduma thabiti na kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja na wadau wetu kulingana na viwango vya ubora wa kimataifa"alisisitiza Bi. Farida

Alisisitiza kuwa, Mamlaka itaendelea kutoa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa ubora ulioanzishwa kulingana na mahitaji ya viwango vyaUbora wa Kimataifa (ISO ).

Kiwango cha ISO 900:2015 ni mfumo wa usimamizi uliotengenezwa na Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO) linalolenga seti ya mahitaji ambayo Taasisi au Shirika linapaswa kufikia katika mfumo wa ubora ili kupata hati ya ISO 9001:2015.




# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI YAIPONGEZA e-GA KWA UBUNIFU

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwan Kikwete (Mb), akitoa taarifa ya Utendaji kazi wa Kituo Cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) mbele ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuendeleza tafiti na bunifu zinazochagiza usanifu na utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA inayoleta tija kwa taifa.

Pongezi hizo zimetolewa Februari 10 mwaka huu na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya PAC Mh. Japhet Hasunga, mara baada ya kamati hiyo kufanya ziara fupi ya kutembelea Kituo Cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kilichopo jijiniDodoma.

Mhe. Hasunga alisema kwamba, e-GA imewezesha serikali kuokoa fedha nyingi kwa kusanifu na kutengeza mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi mbalimbali za umma ambapo, hapo awali mifumo hiyo ilinunuliwa kutoka nje ya Tanzania kwa gharamakubwa.

Mhe. Hasunga alibainisha kwamba, uzoefu unaonesha kuwa katika taasisi mbalimbali za umma walizozitembelea siku za nyuma kulikuwa na changamoto nyingi kuhusu suala la mifumo ya TEHAMA.

“Moja ya jambo lililokuwa linatusumbua sana kamati hii ni taasisi nyingi kununua mifumo ya TEHAMA kutoka nje, lakini msimbo (source code) zinabaki kule kwa waliotengeneza mifumo na wakati mwingine mifumo hiyo baada ya muda haitumiki tena, na hivyo sisi tumekuwa tukisema hakuna thamani ya fedha katika ununuaji wa mifumo hiyo ambayo tumetumia gharama kubwa sana kuinunua,”alifafanua.

Hasunga aliongeza kwamba, licha ya mifumo hiyo kununuliwa kwa gharama kubwa lakini haikuwa na matokeo yaliyotarajiwa hivyo kuziingiza taasisi hizo katika matumizi mabaya ya fedha.

“Kuna taasisi zilinunua mifumo kwa zaidi ya bilioni 30, lakini mfumo haujamaliza mwaka wanautupa, na tulipowauliza walisema waliona mfumo huo haufai hivyo wameamua kutafuta mfumo mwingine,” alibainisha Hasunga.

Aliongeza kuwa katika ziara hiyo kamati ilibaini kwamba, e-GA imesaidia kusanifu na kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA nchini, ambayo imezisaidia taasisi za umma kuokoa fedha nyingi zilizokuwa zinatumika kununua mifumo kutoka nje ya nchi.

> **“Tumefurahi sana kuona namna mifumo mbalimbali inavyowasiliana, tujitahidi tufike angalau asilimia 80, tutakuwa tumefika pazuri kwa sababu tutapunguza gharama na malalamiko katika utoaji wa huduma za serikali mtandao,”**
>
> Mh. Japhet Hasunga
> Makamu Mwenyekiti wa kamati ya PAC



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, akifanya wasilisho kuhusu kituo cha eGOVRIDC kwa kamati ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Katika kuhakikisha mifumo ya TEHAMA Serikalini inawasiliana na kubadilishana taarifa, Hasunga aliitaka e-GA kuhakikisha kwamba taasisi nyingi zaidi zinaunganishwa katika Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB), ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa wananchi.

Naye mjumbe wa kamati hiyo, Mh. Ester Matiko, aliipongeza e-GA na kushauri Serikali kuwekeza zaidi kwa vijana ili kuwezesha nchi kuingia katika teknolojia za kisasa ikiwemo ‘blockchain’ na akili bandia.

“Uwepo wangu hapa nimepata vitu vingi vya ziada ambavyo nilikuwa sivijui, hivyo niiombe Serikali na taasisi zake wawaangalie vijana hawa na wengine ambao wapo huko nje kuhakikisha tunawasaidia na wanatumika ipasavyo katika ujenzi wa Serikali Mtandao,” alisema Matiko.

Kwa upande wake Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh.Ridhiwani Kikwete, aliiomba kamati hiyo kuwa mabalozi wa kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika kuhakikisha inakuza jitahada za Serikali Mtandao nchini.

Pia, Mh. Kikwete aliieleza kamati hiyo kwamba kituo hicho cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao kina eneo finyu hivyo, e-GA inahitaji kutengewa bajeti ili kujenga miundombinu (majengo) yake katika eneo la Kikombo.

“Kituo chetu kinatakiwa kipate nafasi kubwa sana, mmejionea wenyewe maabara zetu ni ndogo sana hivyo serikali (Wizara) itakapoleta bajeti huko bungeni tunaomba mlizingatie jambo hili,” alieleza Kikwete.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, aliishukuru kamati hiyo kutembelea kituo hicho na kuahidi kutekeleza maelekezo, maoni na ushauri uliotolewa na wajumbe wa kamati hiyo ili kuimarisha bunifu na tafiti za Serikali Mtandao




# SIMBACHAWENE: TUTAHAKIKISHA MATUMIZI YA TEHAMA SERIKALINI YANAZIDI KUIMARIKA

Serikali imeahidi kuendelea kusimamia na kuhakikisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma yanaimarika zaidi, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi kidijitali.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh. George Simbachawene, wakati akifungua Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa siku tatu kuanzia Februari 06 hadi 08, mwaka huu katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

"Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2021/22 - 2025/26), kwa pamoja zinatambua nafasi ya TEHAMA katika kufikia malengo ya taifa, na hivyo kusisitiza juu ya matumizi sahihi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kwa umma", alisema Simbachawene.

Aliongeza kuwa, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016, inasisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na yenye tija ya Mifumo ya TEHAMA, katika kuboresha utendaji kazi wa taasisi, unaosaidia kutatua changamoto za kiutendaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kujenga na kuboresha uwezo, pamoja na kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau wa Serikali. Alibainisha kuwa, Wizara yake imepewa dhamana ya kuratibu na kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha dhamira ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan. ya kuijenga Serikali Mtandao inatimia, kwa kuhakikisha huduma zote za Serikali zinapatikana kidijitali na kuwawezesha wananchi kupata huduma hizo kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu mahali walipo.

"Ili kufikia malengo ya kuwa na Serikali Mtandao, Rais ameelekeza kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini, pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, Wizara imetekeleza agizo hili kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kutengeneza Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini ujulikanao kama GoVESB", alisema Simbachawene na kuipongeza e-GA kwa kutekeleza agizo la Rais.

Alisisitiza kuwa, taasisi zote za umma zinapaswa kujiunga kwenye mfumo wa GoVESB ili kubadilishana taarifa kidijitali, kama ambavyo Mhe. Rais amekuwa akisisitiza Taasisi za umma zibadilishane taarifa kidijitali.

"Kama isemavyo kauli mbiu ya kikao kazi hiki "Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Ubadilishanaji Salama wa Taarifa", ni muhimu kuwa na mifumo pamoja na miundombinu ya TEHAMA inayozingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili tuweze kubadilishana taarifa kidijitali na kwa usalama", alisisitiza Mhe. Waziri

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Juma Mkomi, alisema kwamba katika kuhakikisha TEHAMA inaimarika Serikalini, Wizara itaendelea kuboresha miundo ya kiutumishi pamoja na stahiki kwa wataalamu wa TEHAMA ili kuhakikisha wanatumia taaluma zao ipasavyo kuleta matokeo chanya kwa taifa.

"Wizara inatambua kuwa, mafanikio ya Serikali Mtandao ni jumuishi kwa kada zote, niwahakikishie kuwa Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kada zote ili kufanikisha ujenzi wa Serikali ya Kidijitali", alisema Bw.Mkomi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba alisema kuwa, katika utekelezaji wa agizo la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuhakikisha mifumo ya TEHAMA Serikalini inawasiliana na kubadilishana taarifa ambapo, hadi kufikia Januari mwaka huu Taasisi za Umma 109 zimeunganishwa katika mfumo wa GovESB na mifumo 117 imesajiliwa.

Kikao hicho cha siku tatu, kiliwakutanisha takriban wadau zaidi ya 1000 kutoka katika Wizara, Wakala, Idara, Taasisi na Mashirika ya Umma na kujadiliana kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, kuainisha changamoto na kuweka mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto hizo.

# WANAWAKE WAHIMIZWA KUTUMIA TEHAMA KUKUZA UCHUMI




Watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakiwa katika picha ya pamoja

**"Nawaasa wanawake wenzangu tutumie fursa ya uwepo wa TEHAMA ili kukuza uchumi wetu na wa Taifa kwa Ujumla kwani matumizi ya TEHAMA yamerahisisha ufanyaji wa Biashara"**

Bi. Sultana Seiff
Meneja Udhibiti wa Viwango vya Serikali Mtandao

Wanawake nchini, wametakiwa kutumia vema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuongeza vipato vyao na kukuza pato la taifa kwa ujumla.

Wito huo umetolewa na watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Machi 8, mwaka huu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo kitaifa yalifanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Chinangali wilayani Chamwino jijini Dodoma.

Meneja wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff alisema kuwa, kwakuwa TEHAMA ni nyenzo wezeshi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ni vema wanawake wakatumia fursa mbalimbali zitokanazo na TEHAMA ili kujiimarisha kiuchumi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

"Nawasisitiza wanawake wenzangu kutumia TEHAMA katika shughuli zao za kijamii ili kuboresha uchumi wao, kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wao na kuleta tija kwa taifa kwakuwa TEHAMA inatoa fursa nyingi za kiuchumi hivyo ni vizuri tukatambua fursa hizo na kuzitumia kikamilifu kwa ajili ya maendeleo yetu na taifa kwa ujumla", alisisitiza Bi. Sultana.

Kwa upande wake Afisa TEHAMA wa e-GA Bi. Ndili Yusuph alisema kuwa, Mamlaka inatambua mchango wa wanawake kwenye ujenzi wa Serikali ya kidijiti, katika nyanja mbalimbali ikiwemo ulinzi wa mtandao, utengenezaji na uchambuzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA hivyo ni muhimu wanawake wakatumia fursa hiyo kujifunza TEHAMA.

Aliongeza kuwa, kwa sasa dunia ipo katika mapinduzi ya uchumi wa kidijitali ambapo TEHAMA ni nyenzo kuu na inatoa fursa nyingi ambazo wanawake hawana budi kushiriki ili kuisadia nchi yetu iweze kufanikiwa na kupiga hatua katika mapinduzi hayo.

"Nitoe rai kwa wanawake wenzangu hasa wale waliopo shuleni na kazini kujifunza taaluma mbalimbali za TEHAMA ili tuweze kushiriki moja moja katika kukuza jitihada za Serikali Mtandao na vilevile kujiimarisha kiuchumi katika ngazi za familia na jamii zetu", alifafanua Bi. Ndili.

Naye Afisa TEHAMA wa e-GA Bi. Halima Husein, aliwapongeza wanawake wote nchini kwa kuendeleza na kushiriki katika kukuza na kuimarisha jitihada mbalimbali za TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa jamii na kuongeza chachu ya utendaji kazi.

"Wanawake wote tunapaswa kufanya kazi kwa bidii na kutumia fursa zilizopo katika TEHAMA ili kuhakikisha tunaisaida Serikali kuboresha utendaji wake wa kazi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi", alisisitiza Bi. Halima.

Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa Machi 08 kila mwaka ambapo mwaka huu maadhimisho hayo yaliongozwa na kauli mbiu isemayo ***"Wekeza kwa wanawake: Harakisha maendeleo."***




Watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) waliposhiriki katika kuadhimisha siku ya Wanawake Duniani katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma

# WAKUU WA TAASISI ZA UMMA WATAKIWA KUWEKA MAZINGIRA WEZESHI YA UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO



**"Nafahamu kuwa, mmetumia kikao hiki cha siku tatu kujadili changamoto za utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, mmejadiliana pia juu ya mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo na mwisho kabisa mkaweka maazimio, niwapongeze sana na kuwaahidi kuwa, Wizara tumeyapokea maazimio na ushauri mlioutoa na tutaweka mpango mkakati wa kufuatilia utekelezaji wake"**

Mh. Ridhiwani Kikwete (Mb)
Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Wakuu wa Taasisi za Umma wametakiwa kuweka mazingira mazuri na wezeshi ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika taasisi zao ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayoibuka mara kwa mara.

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mh. Ridhiwani Kikwete (Mb), wakati akifunga Kikao Kazi cha Nne cha Serikali Mtandao Februari 08, mwaka huu katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Alisema kwamba, kwakuwa dunia inashuhudia ukuaji na mabadiliko ya teknolojia mara kwa mara, ni lazima Maafisa TEHAMA wapate elimu kuhusu teknolojia mpya kadri zinavyoibuka, ikiwa ni pamoja na namna teknolojia hizo zinavyoweza kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali wakati wote.

"Pamoja na kupata elimu mara kwa mara, ni lazima pia Maafisa TEHAMA katika taasisi zote za umma waendeleze ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kupitia msaada na ushauri wa kiufundi unaotolewa na e-GA, ili sote twende pamoja katika kuijenga Serikali ya Kidijitali", alisema Ridhiwani na kuongeza,

Alibainisha kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria ili e-GA iendelee kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

"Tutakapokuwa tunatekeleza jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao katika taasisi zetu, tuhakikishe pia tunazingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyopo na inayoendelea kutolewa au kuboreshwa mara kwa mara ili kuwa na matumizi salama na sahihi ya TEHAMA Serikalini", alisisitiza Ridhiwani.

Sambamba na hilo, Ridhiwani aliwataka viongozi wa Taasisi za Umma kutatua changamoto za kiutawala zilizo ndani ya uwezo wao ili kuhakikisha watumishi wote wanakuwa katika mazingira salama na rafiki katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Xavier Daudi, aliipongeza e-GA kwa jitihada kubwa inazofanya katika kuimarisha na kukuza matumizi ya TEHAMA Serikalini.

"Kukutana kwa wadau mbalimbali katika kikao kazi hiki kutoka katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, ni moja ya jitihada za e-GA za kukuza Serikali Mtandao kwani, wadau wote mmeweza kukutana kwa pamoja na kujadiliana kuhusu hali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao, changamoto na kuweka mikakati ya kukabiliana nazo", alisema Bw. Xavier.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba, aliwashukuru washiriki wa kikao hicho na kuwataka kuhakikisha miradi na mifumo ya TEHAMA inayojengwa katika Taasisi zao inazingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

"Lengo ni kuhakikisha miradi na mifumo yote ya TEHAMA katika taasisi zetu inarahisisha utendaji kazi, inaboredha utoaji wa huduma kwa umma na kuwezesha mifumo hiyo kusomana na mifumo mingine ya Serikali na kubadilishana taarifa kwa usalama pindi itakapohitajika kufanya hivyo", alisisitiza Ndomba.

Kikao kazi hicho kilichoanza Februari 06 na kuhitimishwa Februari 08 mwaka huu kilibeba kaulimbiu isemayo ***"Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Ubadilishanaji Salama wa Taarifa".***

Kwa taarifa zaidi Skani hapa chini



Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ) Bw. Said Seif Said, akielelezea ushirikiano uliopo kati ya e-GA na e-GAZ

# USHIRIKIANO WA e-GA NA e-GAZ WACHOCHEA MAGEUZI YA KIDIJITALI VISIWANI ZANZIBAR

"Tangu tuliposaini MOU na e-GA tumepiga hatua kubwa sana, mabadiliko yamepatikana na yanaonekana, nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Ndomba kwa uongozi mahiri na timu nzima ya e-GA kwa kuonesha ushirikiano nasi ili kuhakikisha na sisi Zanzibar tunafika kidijitali kwa kuhakikisha mambo mazuri yanatokea bara nasi kwetu pia Zanzibar yanatokea"

Ushirikiano uliopo baina ya Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika ujenzi wa Serikali Mtandao umetajwa kuwa chachu ya mageuzi ya kidijitali visiwani Zanzibar.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa e-GAZ Bw. Said Seif Said, alipotoa salamu za e-GAZ Februari 8 mwaka huu wakati wa hafla fupi ya kufunga Kikao Kazi cha Nne cha Serikali Mtandao kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Alisema kuwa, Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MOU) kati ya e-GA na e-GAZ umeleta mageuzi makubwa ya kidijiti kwa upande wa Zanzibar, kwakuwa taasisi hizo zimekuwa zikifanya kazi kwa ukaribu na kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Serikali Mtandao.

Aliongeza kuwa, Zanzibar inatarajia kuanza kutumia mfumo wa e-Vibali ambapo kwa sasa e-GA inashirikiana na e-GAZ kuhakikisha mfumo huo unaweza kutumika visiwani humo kwakuwa tayari unatumika bara na umeleta mafanikio makubwa tangu ulipoanza kutumika.

"Wiki hii tulikuwa na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar na moja kati ya jambo lililoonekana zuri na kumfurahisha kiongozi huyo ni namna tunavyoshirikiana na wenzetu e-GA kuhakikisha mfumo huu wa e-Vibali unatumika pia Zanzibar, naomba niwafikishie salamu za Katibu Mkuu Kiongozi anashukuru na kuwapongeza sana e-GA, kwakuwa mmekuwa si wachoyo kwa yale mazuri mnayokuwa nayo mnahakikisha nazi Zanzibar pia tunakuwa nayo", alisema Bw. Said.

Alisema kuwa, e-GA imekuwa ikitoa msaada wa karibu kwa e-GAZ kuhakikisha ujenzi wa Serikali Mtandao unafanikiwa kwa upande wa Zanzibar ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na kuhakikisha wananchi wanapata huduma za serikali kwa haraka na gharama nafuu mahali walipo.


Alibainisha kuwa, makubaliano ya ushirikiano huo yamesaidia kuleta mabadiliko makubwa katika utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika utekekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali Visiwani Zanzibar.

Aliyataja baadhi ya makubaliano ya ushirikiano kuwa ni pamoja na kusaidiana kitaalamu, kushauriana na kupeana mafunzo baina ya wataalamu wa taasisi hizo mbili ambapo mashirikiano haya yamewezа kuonekana katika utengenezaji na uimarishaji wa mifumo mbalimbali.

Aidha, Bw. Said aliipongeza Mamlaka kwa juhudi zilizofanyika na kwa ushirikiano unaoendelea kutolewa wa kuhakikisha Zanzibar inafikia mapinduzi ya uchumi wa kidijitali ikiwemo juhudi za kuhakikisha mfumo wa vibali vya kusafiri nje ya nchi (e-vibali) unatumika Zanzibar.

"Napenda kuwafikishia pongezi na salamu kutoka kwa Katibu Mkuu Zanzibar ambaye amefurahishwa sana kwa jitihada zilizofanyika za kuhakikisha mfumo wa e -vibali unatumika Zanzibar" alisisitiza Bw. Said.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba, alisema kuwa e-GA itaendeleza ushirikiano mzuri uliopo na e-GAZ ili kuhakikisha mapinduzi ya TEHAMA Serikalini yanaimarika katika pande zote mbili za muungano na kuwawezesha wananchi kupata huduma bora na rahisi wakati wote mahali walipo.





Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani Bw. Suleiman Zalala, akitoa salamu za Shukrani wakati wa kilele cha Kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao

# USHIRIKISHWAJI WA WATU WENYE ULEMAVU WACHANGIA UBORESHAJI WA HUDUMA JUMUISHI

Ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika makongamano na mikutano ya kitaaluma, umetajwa kuwa chachu ya uboreshaji wa huduma jumuishi kwa makundi maalumu.

Hayo yameelezwa na Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani Bw. Suleiman Zalala, alipotoa salamu za shukurani wakati wa kilele cha Kikao Kazi cha Nne cha Serikali Mtandao kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) uliopo jijini Arusha Februari 8 mwaka huu.

Aliongeza kuwa, ni wakati sahihi kwa Taasisi nyingine za Umma na binafsi kutowaacha nyuma watu wenye ulemavu kwa kuiga mfano mzuri wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wa kuhusisha makundi maalumu kwenye makongamano pamoja na mafunzo mbalimbali wanayoyaandaa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Eng. Benedict Ndomba, aliahidi kuendeleza ushirikiano na makundi maalumu ikiwemo CHAVITA, ili kuhakikisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao unachagiza maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa makundi yote muhimu ya kijamii.

Alibainisha kuwa, e-GA itaendelea kushirikiana na makundi maalum sambamba na kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ili kuhakikisha Serikali Mtandao inaleta manufaa kwa watu wote wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu.

"Serikali Mtandao inalenga kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi mahali walipo na kwa gharama nafuu sisi e-GA tunadhamiria kuhakikisha makundi yote ya kijamii wakiwemo walemavu wananufaika na Serikali Mtandao", alisema Ndomba.

Kikao Kazi cha Nne cha Serikali Mtandao kiliongozwa na kaulimbiu isemayo uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Ubadilishanaji Salama wa Taarifa na kuwakutanisha takribani Zaidi ya wadau 1000 kutoka katika Taasisi, na Mashirika ya Umma.

**"Huu ni mwaka ya pili tunashiriki katika kikao cha aina hii, e-GA imetuthamini kwakuona umuhimu na mchango wa kundi hili maalumu kushiriki katika kikao kazi cha Nne cha Serikali Mtandao, ili kupata nafasi ya kukutana na wadau mbalimbali wa TEHAMA sambamba na kuwasilisha changamoto tulizonazo na mahitaji yetu ili kuboresha huduma jumuishi za Serikali Mtandao kwa watu wenye ulemavu"**




Washiriki wa Kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kutoka katika Taasisi Mbalimbali za Umma wakifuatilia kwa makini mada zilizowasilishwa katika kikao hicho.

# WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WATUMISHI WA e-GA KUENDELEA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA UADILIFU



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mhe. George B. Simbachawene (Mb), akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao wakati alipofanya ziara katika ofisi za e-GA tawi la Iringa

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mh. George Simbachawene, amewataka watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuendelea kufanya kazi kwa ubunifu na uadilifu, ili kuhakikisha dhamira ya ujenzi wa Serikali Mtandao inatimia. Waziri Simbachawene aliyasema hayo jana baada ya kutembelea Ofisi za e-GA kituo cha Iringa na kufanya mazungumzo na watumishi wa kituo hicho.

Alibainisha kuwa, dhamira ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan, ni kuona huduma kwa wananchi zinakuwa bora na kupatikana kwa urahisi zaidi kupitia TEHAMA.

"Wengi wenu hapa ni vijana wadogo, tuna imani kubwa nanyi katika kuhakikisha ufanisi wa utendaji kazi Serikalini unaimarika na wananchi wanapata huduma kwa urahisi na gharama nafuu mahali walipo kwa njia ya kidijitali, hivyo muendelee kuwa wabunifu lakini uadilifu uwe ngazi yenu katika kuisaidia Serikali kwenye mageuzi haya", alisema Simbachawene.

Katika ziara hiyo Waziri Simbachawene aliongozana na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb)

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba, alimshukuru Waziri Simbachawene kwa kutembelea kituo hicho na kutoa maelekezo yatakayosaidia kuboresha utendaji kazi wa kituo hicho




Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakimsikiliza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mhe. George B. Simbachawene(Mb), wakati alipofanya ziara katika ofisi za e-GA tawi la Iringa

# WATAALAMU WA TEHAMA SERIKALINI WAPEWA MAFUNZO

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeratibu na kuendesha mafunzo ya uchambuzi wa Data kubwa 'Big data analysis' na Akili Mnemba 'Artificial intelligence-AI', kwa wataalam wa TEHAMA kutoka katika Taasisi mbalimbali za Umma, ili kukuza na kuwajengea uelewa wa pamoja kuhusu teknolojia hizo utakaosaidia kukuza ufanisi na kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo hayo Machi 23 mwaka huu, Meneja Usimamizi wa Usalama wa TEHAMA (e-GA) Bw.Riziki Majengo alisema, mafunzo hayo yanaendeshwa na e-GA ikiwa ni utekelezaji wa kifungu cha 5(2)(h) cha Sheria ya Serikali Mtandao Namba 10 ya Mwaka 2019, kinachoielekeza e-GA kuzijengea uwezo Taasisi za Umma katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Abainisha kuwa, miongoni mwa faida za mafunzo hayo kwa Taasisi za umma ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kusaidia kuboresha mifumo ya ndani ya nchi kwa kutumia teknolojia hizo.

Aliongeza kuwa, mafunzo hayo yameendeshwa kwa vitendo Zaidi na hivyo kuwapa washiriki muda wa kutosha wa kujifunza na kuelewa vema kuhusu 'Big data analysis' na 'Artificial Intelligence' pamoja na matumizi yake katika mazingira na mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Aidha, washiriki wa mafunzo hayo wameipongeza e-GA na kueleza kufurahishwa na mafunzo hayo ambayo yamewajengea uwezo kuhusu matumizi ya teknolojia hizo na kuahidi kutumia elimu waliyopata kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Kwa upande wake Afisa TEHAMA kutoka Tume

**'Tayari tuna mifumo na miundombinu mbalimbali ya kukusanya hizi taarifa nyingi, kwahiyo baada ya mafunzo haya tunaenda kuongeza ubora zaidi kwenye mifumo yetu kwa kutumia Akili mnemba 'Artificial Intelligence' ili kufanya mashine kufikiria na kufanya maamuzi mengi zaidi ambapo itasaidia kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa utoaji huduma kwa wananchi"**

**Bw.Riziki Majengo**
Meneja Usimamizi wa Usalama wa TEHAMA (e-GA)

ya Mipango Bw.Godhard Hunja alisema kuwa, mafunzo hayo yataleta tija kubwa katika taasisi yake kwani yatasaidia katika uchambuzi wa takwimu mbalimbali kutoka kwenye taasisi zinazotekeleza miradi ya maendeleo, jambo ambalo litasaidia kupata majibu yenye tija na kuweza kushauri vyema namna ya kuendelea na utekelezaji wa miradi kulingana na takwimu zilizopokelewa.

Naye Meneja wa Oparesheni Kituo cha Taifa cha kuhifadhi Data (NIDC) Bi. Nasra Mugheiry ameipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuwakusanya wataalam kutoka taasisi mbalimbali za umma na kuwapa elimu hiyo muhimu ambayo imekuwa ikitumika katika nchi zilizoendelea

''Big data analysis na Artificila intelligence hizi ni teknolojia muhimu sana kwa dunia ya sasa na tayari zinatumiwa na nchi zilizoendelea, kwaiyo sisi kupewa mafunzo haya yatakwenda kuongeza motisha na ujuzi kwa wafanyakazi na pia kuiwezesha serikali kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi'', alisema Nasra.

Mafunzo hayo ni ya awamu ya pili katika mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo awamu ya kwanza ilifanyika Januari 29 hadi Februari 17 mwaka huu na yalihusisha jumla ya wataalamu 20 kutoka katika Taasisi za Umma 10 na awamu ya pili imefanyika Machi 4 hadi 23 mwaka huu na kuhusisha wataalamu 23 kutoka taasisi za umma 15 na hivyo kufanya jumla ya wataalamu waliopatiwa mafunzo hayo kuwa ni 43 kutoka Taasisi za Umma 25, mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere kilichopo Kibaha mkoani Pwani katika awamu zote mbili.





Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali za Umma wakifuatilia kwa makini mafunzo ya uchambuzi wa Data kubwa 'Big data analysis' na Akili Mnemba 'Artificial intelligence-AI' .Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watumishi hao katika maeneo ya Big Data Analysis na Artifical Intelligence

# WATUMISHI WA e-GA WATAKIWA KUJIEPUSHA NA RUSHWA

Afisa Uchunguzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Bi. Dorothea Mrema, amewataka watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuzingadia uadilifu na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ili kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Bi Dorothea alitoa kauli hiyo Januari 6 mwaka huu, wakati akitoa elimu kuhusu rushwa mahala pa kazi kwa watumishi wa e-GA, kwenye mkutano wa watumishi hao uliofanyika katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa, watumishi wa umma wanapaswa kushiriki mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU, pale wanaposhuhudia uwepo wa viashiria au vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Aliongeza kuwa, TAKUKURU inatambua mchango wa TEHAMA katika kuzuia rushwa ikiwa ni pamoja na uwepo wa mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya utoaji wa huduma kwa wananchi, ambayo imechangia kuimarisha utoaji wa huduma na kupunguza mianya ya rushwa.

"Tunaipongeza e-GA kwa kutengeneza mifumo mbalimbali ya kielektroniki inayorahisisha utendaji kazi wa serikali na utoaji wa huduma kwa umma, lakini pia mifumo hii imesaidia kupunguza mianya ya rushwa kwa asilimia kubwa tofauti na awali", alifafanua Bi. Dorothea.

Alibainisha kuwa, ni vema kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusu uwepo na upatikanaji wa huduma za Serikali kupitia mifumo ya kielektroniki iliyopo sambamba na kuendelea kuiboresha zaidi ili wananchi waweze kupata huduma bora na kuondoa mianya yote ya rushwa.

Aidha, Bi. Dorothea ametoa rai kwa wanachi ikiwa ni pamoja na watumishi wa umma na wanafunzi, kujiunga katika vikundi (klabu) mbalimbali za mapambano dhidi ya rushwa ili kupata uelewa zaidi na kufahamu mikakati mbalimbali itakayosaidia katika kuondoa rushwa nchini.

**"Tunaipongeza e-GA kwa kutengeneza mifumo mbalimbali ya kielektroniki inayorahisisha utendaji kazi wa serikali na utoaji wa huduma kwa umma, lakini pia mifumo hii imesaidia kupunguza mianya ya rushwa kwa asilimia kubwa tofauti na awali"**



Afisa Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Bi. Dorothea Mrema, akiwasilisha mada wakati wa kikao cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).



Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakisikiliza kwa makini mada mbalimbali zilizotolewa wakati wa kikao cha watumishi kilichofanyika Jijini Dar Es Salaam mapema mwaka huu



# ONGEZEKO LA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZA TISHIO KWA WATUMISHI WA UMMA

Afisa anayeratibu Afua za VVU mahali pa kazi ngazi ya taifa, katika sekta ya umma kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Hafidh Ameir, akitoa mada kuhusu magonjwa sugu yasiyoambukiza wakati wa kikao cha Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

> **"Hakikisheni mnapokuwa kazini msikae zaidi ya saa moja bila kufanya mazoezi ya kutembea, ni vizuri kujenga utaratibu huu ili kuruhusu mzunguko wa damu katika mwili hii itawasaidia kuepukana na magonjwa sugu yasiyoambukiza,"**

Kundi kubwa la watumishi wa umma, lipo katika hatari ya kupata magonjwa sugu yasiyoambukiza kutokana na mwenendo wa maisha usioridhisha ikiwa ni pamoja na kutokuwa na tabia ya kufanya mazoezi na ulaji usiozingatia mpangilio sahihi wa lishe.

Hayo yamebainishwa na Afisa anayeratibu Afua za VVU mahali pa kazi ngazi ya taifa, katika sekta ya umma kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Hafidh Ameir, wakati akitoa elimu kuhusu VVU, UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza kwa watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Januari 06 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa, watumishi wa umma wapo katika hatari kubwa ya kupata magonjwa yasiyoambukiza ukiwemo ugonjwa wa shinikizo la damu na sukari, hali inayosababishwa na watumishi kutokuwa na utaratibu wa kufanya mazoezi mara kwa mara pamoja na ulaji wa vyakula usiozingatia lishe bora.

"Asilimia kubwa ya watumishi wanafanya kazi zinazowalazimu kukaa muda mrefu wawapo kazini, lakini pia wengi hawana utaratibu wa kufanya mazoezi na hutumia vyakula vya viwandani (junk foods), hali inayopelekea wengi wao kupata magonjwa sugu ikiwemo shinikizo la damu, sukari, ugonjwa wa ini n.k", alifafanua Dkt. Hafidh.

Ili kukabiliana na magonjwa hayo, Dkt. Hafidh amewashauri watumishi wa e-GA kupunguza muda wa kukaa kwa kufanya mazoezi mepesi ya kutembea dakika chache kila baada ya saa moja wanapokuwa kazini, ili kuruhusu damu kuzunguka mwilini.

Kwa upande mwingine Dkt. Hafidh aliwataka watumishi wa e-GA kulinda afya zao dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kujiepusha na ngono zembe, kutumia kinga pamoja na kuwa na utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara na kupata ushauri wa kitaalamu.

"Wengi wenu hapa ni vijana, mnapaswa kufahamu kuwa UKIMWI bado upo na sote tunapaswa kuchukua tahadhari ya kujilinda na ugonjwa huu, ni lazima vijana mkubali kuacha ngono zembe, mtumie kinga na kujenga utaratibu wa kupima afya zetu sambamba na kufata ushauri wa daktari mtakaopewa" alisisitiza Dkt. Hafidh.

Naye Kaimu Meneja Mafunzo kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) Bw. Erick Mororo, aliwataka viongozi wa e-GA kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi ili kuongeza ufanisi kwa watumishi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Alisema kuwa, waajiri wanawajibu wakuzingatia maelekezo yanayotolewa na OSHA ikiwemo kuzingatia usalama na afya mahali pa kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa watumishi.

"Kila mtendaji katika Taasisi anapaswa kulinda afya za watumishi wake dhidi ya athari hasi, magonjwa na vifo vinavyoweza kutokea kazini kwa kuhakikisha anaweka mazingira salama kuanzia vifaa vinavyotumika ofisini kama vile viti, usafi wa mazingira nk", alifafanua.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba, alisema kuwa Mamlaka itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watumishi ili kuhakikisha usalama wa afya ya akili na mwili wanapokuwa kazini.

Katika mapambano dhidi ya UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza, Ndomba alisema kuwa, Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kupitia programu mbalimbali pamoja na kuwawezesha kushiriki katika michezo ili kuimarisha afya ya akili na mwili.




Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakifurahia mada zilizokuwa zikitolewa wakati wa kikao cha watumishi kilichofanyika Jijini Dar Es Salaam mapema mwaka huu.



Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakifurahia mada zilizokuwa zikitolewa wakati wa kikao cha Watumishi kilichofanyika Jijini Dar Es Salaam mapema mwaka huu.

# TENGENI MUDA WA MAISHA BINAFSI KUEPUKA UGONJWA WA AFYA YA AKILI



Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili Dkt. Garvin Kweka, akiwasilisha mada kuhusu Afya ya Akili wakati wa kikao kazi cha Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). wametakiwa kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya masuala mbalimbali yanayohusu maisha binafsi, ili kujiepusha na msongo wa mawazo unaoweza kusababisha matatizo ya afya ya akili.

Wito huo umetolewa Januari mwaka huu na Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili Dkt. Garvin Kweka, wakati akitoa elimu ya afya ya akili kwa watumishi wa Mamlaka katika kikao cha watumishi kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Dkt. Kweka alisema kuwa, katika tafiti zilizofanywa na wanasayansi wa afya ya akili, zimebaini kuwa, sababu kubwa za watu wanaojitoa uhai zinatokana na mahusiano mabovu au hafifu na jamii zao na hivyo kupelekea kuchukua maamuzi yasiyokuwa sahihi.

"Ni muhimu kutenga muda kwa ajili ya familia na jamii ili kuweza kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza badaye ikiwemo msongo wa mawazo na hatimaye kupelekea kujiua, ni vizuri kuhakikisha kila mmoja wetu hapa anakuwa na mahusiano mazuri na muda wa kutosha na familia pamoja na jamii yake inayomzunguka", alisema Dkt. Kweka.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa watumishi kuweka uwiano sawa wa maisha binafsi na ya kazini ili kuweza kujiepusha na matatizo ya afya ya akili nayoweza kujitokeza kutokana na kutokuwepo kwa uwiano sawa wa Maisha ya kazini na binafsi.

"Binadamu ukimfungia ndani unambadilisha hali ya afya yake ya akili anapata mihemko isiyokuwa sahihi, hivyo ili kuweza kukabiliana na msongo wa mawazo mahusiano na jamii ni sehemu muhimu ya afya ya akili" Alisisitiza Dkt. Kweka

Naye Mkaguzi wa ndani wa Mamlaka ya Serikali Mtando Bw. Christopher Kambo alisema kuwa, elimu ya afya ya akili iliyotolewa na mtaalamu huyo, imewasaidia kutambua umuhimu wa kuchangamana na jamii ili kuweza kujiepusha na matatizo ya afya ya akili ikiwemo msongo wa mawazo.

Bw. Kambo alisema kuwa, asilimia kubwa ya watumishi katika maeneo mbalimbali wamekuwa wakitumia muda wao mwingi kutekeleza majukumu ya kikazi na hivyo kusahau kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya familia na jamii jambo linaloweza kusababisha msongo wa mawazo.

"Elimu tuliyopewa kuhusu afya ya akili imetusaidia kutambua na kuweka uwiano sawa wa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi na maisha binafsi, lakini pia namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku ya kikazi", alisisitiza Bw. Kambo.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imekuwa na utaratibu wa kutoa elimu ya afya ya akili kwa watumishi wake mara kwa mara ili kuhakikisha wanapata elimu sahihi juu ya magonjwa mbalimbali ukiwemo ugonjwa wa afya ya akili ili waweze kuuzuia au kukabiliana nao katika hatua za awali kabla haujaleta madhara.

# MIAKA 3 YA RAIS
## DKT. SAMIA: SERIKALI MTANDAO YAZIDI KUIMARIKA



Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ilianza siku na hatimaye miaka mitatu sasa imetimia tangu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuingia madarakani.

Ilikua Ijumaa ya Machi 19 mwaka 2021, siku ambayo historia iliwekwa kwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuapishwa rasmi na Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanza kuongoza rasmi Serikali ya Awamu ya Sita.

Siku hii ilikuwa ya kihistoria kwa Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na Rais wa kwanza mwanamke na jemedari mahiri ambaye anaijenga Tanzania mpya ya Kididjitali, anaweka vipaumbele mbalimbali vya kitaifa kwa maendeleo ya nchi, anasisitiza uzalendo, analeta umoja na mshikamano, anaimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo pamoja na kufanya kazi kwa bidii.

Katika kuhakikisha dhamiria ya ujenzi wa Serikali ya Kidijitali, moja ya vipaumbele alivyoviweka Mhe. Rais, Dkt Samia ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini kwa kuhakikisha TEHAMA inatumika kwenye utendaji kazi ili kuongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa wananchi.

> "Matumizi sahihi na salama ya TEHAMA, ni muhimu katika dunia ya sasa ili kupunguza mianya ya rushwa. kuboresha utoaji wa huduma kwa umma na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Serikali", hii ni moja ya kauli ya Mhe. Rais ambayo amekuwa akisisitiza dhamira yake ya kujenga Serikali ya kidijitali. "



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict B Ndomba ,akitoa ufafanuzi wa namna ambavyo Serikali ya awamu ya sita (6) imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya TEHAMA Serikalini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict B. Ndomba, anasema kuwa kumekuwa na mafanikio chanya katika matumizi ya TEHAMA Serikalini, ambayo yamechochewa na utayari wa Serikali ya awamu ya sita.

"Kutokana na uongozi bora wa awamu ya sita, Mamlaka imefanikiwa kujenga, kuboresha na kusimamia uendeshaji wa Vituo vya Serikali vya Kuhifadhi Mifumo na Taarifa (Government Data Center), ambapo hadi sasa vituo hivyo vinatumiwa na zaidi ya taasisi 121 kuhifadhi Mifumo na tarifa zao kwa usalama wa uhakika, ujenzi na usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GOVNET) ambapo hadi sasa Taasisi zaidi ya 299 zimeunganishwa na kuwezeshwa kuwasiliana chini ya uratibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao", anafafanua Mhandisi Ndomba.

Katika kufikia malengo hayo, Mhe. Rai amekuwa akisisitiza uwepo wa mifumo ya TEHAMA ambayo inawasiliana na kubadilishana taarifa ili kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wananchi unaimarika, ambapo e-GA imesanifu na kutengeneza Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji taarifa Serikalini ujulikanao 'Government Enterprise Service Bus-GoVESB'

Aidha, Meneja wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA wa e-GA Bw. Abdallah Samizi, anasema kuwa e-GA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma kwa kutengeneza na kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA ukiwemo mfumo wa GoVESB.

Mfumo wa GoVESB, ni moja ya maelekezo ya Mhe. Rais ya kuhakikisha mifumo ya Serikali inawasiliana na kubadilishana taarifa lakini pia, ni utekelezaji wa Kifungu na. 48 cha Sheria ya Serikali Mtandao Namba. 10 ya Mwaka 2019 ambacho kinaielekeza Mamlaka kutengeneza Mfumo shirikishi unao wezesha mifumo ya Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma imesanifu na kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na Mfumo wa e-Mrejesho ambao unawawezesha wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Taasisi za umma kwa njia ya kidijitali, ili kuwasilisha maoni, mapendekezo, maswali, pongezi au malalamiko yao sambamba na kufuatilia utekelezaji wake ndani ya Taasisi husika.

Mifumo mingine ni pamoja na Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-office) unaorahisisha shughuli za mzunguko wa mafaili na nyaraka ndani ya Taasisi za Umma, Mfumo wa e-Board unaowezesha uratibu wa shughuli zote za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma.

Vilevile, Mfumo wa e-Mikutano unawawezesha watumishi wa Taasisi za Umma kufanya vikao kidijitali mahali walipo bila kulazimika kukutana mahali pamoja na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uandaaji na uendeshaji wa vikao, mfumo e-Dodoso unaomuwezesha mwananchi au taasisi kutengeneza na kujaza dodoso, kupata tathmini pamoja na takwimu za dodoso kwa njia ya mtandao.

**"Mamlaka imetengeneza mfumo wa m-GOV, ambao ni mfumo jumuishi wa utoaji wa huduma za Serikali kwa njia ya simu za mkononi unaorahisisha na kuharakisha utoaji wa huduma kwa umma, mfumo huu umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mkononi nchini Tanzania na unatoa huduma za ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) ,kwa kutoa na kupokea taarifa kupitia namba jumuishi 15200 na 15201 pamoja na huduma za menyu ya namba ya msimbo (USSD) kupitia namba jumuishi *152*00#",**

Bw. Abdalla Samizi
Meneja Utengenezaji Mifumo


GOVERNANCE

GOVERNANCE

EQUITABLE GROWTH, FINANCE & INSTITUTIONS INSIGHT

GovTech Maturity Index

2022 Update

Trends in Public Sector Digital Transformation

December 2022

Public Disclosure Authorized

Supported by the GovTech Global Partnership (GTGP) and the KDI School (Republic of Korea)



Bi. Sultana Seiff Meneja Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao anasema, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya awamu ya sita, Mamlaka imekuwa ikifanya vikao mbalimbali vya kiufundi na Taasisi za Umma kwa lengo la kutoa msaada, ushauri na elimu juu ya uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Aidha, takribani nyaraka zaidi ya 263 za TEHAMA zimewasilishwa kutoka Taasisi mbalimbali za umma ili kufanyiwa mapitio na kupata ushauri wa kiufundi na maboresho kupitia Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini (GISP) ambayo ni dirisha moja la huduma za TEHAMA Serikalini yenye lengo la kuhakikisha uwepo wa usimamizi bora wa miradi ya TEHAMA, utoaji wa huduma bora na ushirikishwaji wa taasisi za umma kwa ufanisi.

Ripoti ya utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (WB) kuhusu ukomavu wa matumizi ya Teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi (GovTech Maturity Index) uliofanyika mwaka 2022 katika nchi 198 duniani, inabainisha kuwa Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazopiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA kwa kushika nafasi ya 26 kidunia na ya pili barani Afrika nay a kwanza Afrika Mashariki.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa, mafanikio hayo yanatokana na utayari wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, uwepo wa dira mahususi kuhusu sera ya TEHAMA, Sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, mikakati madhubuti na utekelezaji wake unaosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

# KUTOKA KITUO CHA UTAFITI NA UBUNIFU - eGOVRIDC



## Fahamu kuhusu eBarua

HAKUNA mtandao!!!?, hakuna tatizo kazi iendelee! Hii ndiyo kauli unayoweza kusema ukiwa unatumia toleo jipya la baruapepe za serikali (GMS Client) ambayo inachagizwa na jina jipya la e-Barua.

Mfumo huu uliobuniwa na kusanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) umeingia katika maboresho muhimu katika kujibu changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwa watumiaji wake ambao ni watumishi ndani ya Wizara,Halmashauri na Taasisi za Umma.

Moja ya changamoto iliyopatiwa majibu katika toleo hili jipya,ni uwezo wa mtumiaji kusoma na kutumia barua pepe zake bila kuwa na mtandao wa intaneti(offline mode), hii ni hatua kubwa katika mapinduzi ya serikali mtandao nchini.

Kwa mujibu wa Meneja wa Kituo cha Utafiti,Ubunifu,Mafunzo na Maendeleo ya Serikali Mtandao Dkt.Jaha Mvulla amesema maboresho katika mfumo wa barua pepe za serikali yamefanyika ili kurahisha utendaji kazi na kuboresha huduma kwa wananchi.

Dkt.Mvulla amesema maboresho yaliyofanyika katika mfumo wa barua pepe za serikali yamepelekea kuzaliwa kwa nadharia ya e-Barua ambayo ni suluhu kwa baadhi ya changamoto zilizokuwa zinajitokeza huko nyuma katika baruapepe za serikali.

"Moja ya changamoto ilikuwa ni mtumishi kushindwa kusoma tena email (baruapepe) zake ambazo tayari alishazifungua lakini anataka kupitia upya ujumbe uliondikwa, kwa mfumo wa baruapepe za kawaida hauwezi kuzifungua,ni lazima uwe na mtandao,lakini mfumo wa e-Barua utaweza kuzisoma hata usipokuwa na mtandao." Amefafanua Dkt.Mvulla.

Pia,Dkt.Mvulla ameongeza kwamba watumiaji wa e-Barua wataweza kutuma baruapepe hata wakiwa katika mazingira ambayo hayana mtandao kabisa na ujumbe huo utahifadhiwa,na kifaa chake kitakapokuwa kwenye eneo lenye mtandao barua au ujumbe huo utatumwa.

Sanjari na hilo, Meneja huyo ameeleza kwamba e-Barua imeanza kufanya kazi kwa majaribio (pilot) katika matoleo mbali ikiwemo kwenye programu tumizi za simu (mobile application) pamoja na toleo la kompyuta za mezani (desktop).

Pamoja na sifa hizo kuu,Dkt.Mvulla ameeleza kwamba mfumo wa e-Barua una uwezo wa kutuma taarifa (notification) kwa mtumiaji kuhusu kuingia kwa ujumbe mpya katika anuani yake ya baruapepe.



"Kutumia mfumo huu pia unaweza ukapanga baruapepe yake itumwe muda gani, hivyo utaandika na kupanga muda wako na itajituma muda ukifika Kwenda kwa mlengwa.

Kwa upande wa usalama wa mfumo huu, viwango vya kimataifa katika kulinda faragha za mtumiaji za kazi zake akiwa mkondoni vimezingatiwa.hivyo katika mfumo wa e-Barua mtumiaji hatotumia tena nywila ili kuingia kwenye mfumo.

Mfumo wa e-Barua utatumia zaidi alama za kibayometriki (alama za vidole na utambuzi wa sura ) ili kuweza kufungua na kutumia mfumo huu wa kisasa zaidi katika historia ya Serikali Mtandao nchini.

Kwa mujibu wa Bw.Darwin King'ani Afisa TEHAMA e-GA amebainisha kwamba hatua hiyo itaimarisha ulinzi kwa mtumiaji kwa kiwango cha juu zaidi.

"Ili e-Barua ifunguke ni lazima itambue alama zako za vidole au sura,tofauti na mfumo wa zamani ambao ulikuwa unatumia nywila ambayo mtu mwingine anaweza inakiri au ikariri kisha akatumia kuingia na kufanya mawasiliano kinyume na matakwa au ridhaa ya mhusika." Amefafanua Bw.King'ani.

Mtaalamu huyo wa TEHAMA amebainisha kwamba katika hatua za awali za maendeleo ya ubunifu ya mfumo huu kila mtumiaji atatakiwa kuwa na simu ya mkononi yenye uwezo wa kutambua alama za kibailojia yaani 'biometric' ambapo baada ya kujisajili ndiyo ataweza pia kujiunga na kompyuta ya mezani.



**Dkt.Jaha Mvulla**
**Meneja - eGOVRIDC**

# MATUKIO KATIKA PICHA

## YALIYIJIRI KATIKA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO FEB 6-8, 2024 AICC ARUSHA




Waziri Wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (katikati), akiwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - UTUMISHI Bw. Juma Mkomi (kulia kwake) na Mkuu wa Wilaya ya Karatu Mhe. Dadi Kolimba aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao wakiwasili katika ukumbi wa AICC kwa ajili ya kushiriki kikao hicho.



Mhe. Waziri George Simbachawene (Mb), akisalimiana na viongozi mbalimbali mara baada ya kuwasili katika viwanja vya AICC.




Mhe. Waziri George Simbachawene (Mb), akitoa hotuba kwa washiriki wa kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.






Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb), akitoa hotuba kwa washiriki wa kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.



Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA) Dkt. Jasmine Tiisekwa, akitoa salamu kwa washiriki wa Kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.



Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bw. Selestine Gervas Kakele, akizungumza wakati wa kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.



Katibu Mkuu - UTUMISHI Bw. Juma Selemani Mkomi, akifuatilia mada mbalimbali wakati wa Kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba, akiwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao wakati wa Kikao cha 4 cha Serikali Mtandao.

# Baadhi ya watoa Mada wa kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao wakiwasilisha Mada hizo katika ukumbi wa AICC



Bw. Erick Kitali
Mkurugenzi wa TEHAMA - Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).



Bw. Sylvan Shayo
Mkurugenzi wa Udhibiti wa Viwango, Miongozo na Usalama wa TEHAMA (e-GA).



Bw. Raymond Machary
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).



Bw. Bernard Konga
Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).



Dkt. John Sausi
Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha - Wizara ya Fedha



Bw. Ibrahim Toure
Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za TEHAMA Serikalini, Sehemu ya Sera na Viwango

# Waziri Wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb), akitoa zawadi na vyeti mbalimbali kwa wadhamini wa kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.














eGA


eGA


eGA


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange."
eGA


Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data
eGA


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange."
eGA


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange.”
eGA


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange.”
eGA


eGA
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange.”
Certificate


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Certificate


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange.”
eGA


THE 4TH e-GOVERNMENT ANNUAL MEETING
eGA
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT

# KIKAO CHA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) NA WAKUU WA TAASISI ZA UMMA KUHUSU JITIHADA ZA UKUZAJI WA SERIKALI MTANDAO

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, akiongoza kikao cha Wakuu wa Taasisi za Umma kilichojadili mambo mbalimbali yanayohusu ukuzaji wa Serikali Mtandao



**Mhandisi Benedict Ndomba**
**Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).**





**Dkt. Jabiri Kuwe**
**Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).**



**CP. Salum R. Hamduni**
**Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).**



Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Umma wakifuatilia kikao cha wakuu wa Taasisi za Umma



**Bw. Selestine Kakele**
**Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**



**Bw. Firimin Msiangi**
**Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za taifa.**



**Bi. Justina Mashiba**
**Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).**



**Bw. Priscus Kiwango**
**Mkurugenzi wa TEHAMA Serikalini**

# HAFLA YA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 8 FEBRUARI 2024




Naibu Waziri Ofisi Ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwan Kikwete akifunga kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao




Naibu Waziri Ofisi Ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwan Kikwete (kushoto) akiteta jambo na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba wakati wa hafla fupi ya kufunga kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.



Washiriki wa kikao kazi cha 4 cha Serikali cha Serikali Mtandao wakipiga makofi kupongeza mada zilizokuwa zinatolewa wakati wa kikao hicho.




Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA) Dkt. Jasmine Tiisekwa, akitoa salamu wakati wa hafla ya kufunga kikao kazi cha 4 cha Serikali Mtandao tarehe 8 Februari mwaka huu katika ukumbi wa AICC jijini Arusha



Washiriki wa kikao kazi cha 4 cha Serikali cha Serikali Mtandao wakipiga makofi kupongeza mada zilizokuwa zinatolewa wakati wa kikao hicho



Naibu Waziri Ofisi Ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwan Kikwete (kushoto) akipokea maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhe. Benedict Ndomba wakati alipotembelea banda la e-GA




Meneja wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff akisoma majina ya taasisi za Umma zilizofanya vizuri katika uzingatiaji wa viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa mwaka wa fedha 2023/2024




Naibu Waziri Ofisi Ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwan Kikwete akipokea maelezo kutoka kwa watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao alipotembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao katika Viwanja vya AICC jijini Arusha.

# WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA MHE. GEORGE SIMBACHAWENE ALIPOTEMBELEA MABANDA MBALIMBALI YA MAONYESHO WAKATI WA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO













# WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA MHE. GEORGE SIMBACHAWENE AKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA MAKUNDI MBALIMBALI YA WASHIRIKI WA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO










BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
"Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange."


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
"Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange."


BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT
"Ensuring Compliance to e-government Policies, Laws, Standards and guidelines for Secure Electronic Data Exchange."


KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO
MGENI RASMI:
Mhe.GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT


MGENI RASMI:
Mhe.GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
6-8 Februari,2024
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT


MTANDAO
MGENI RASMI:
Mhe.GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
6-8 Februari,2024
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT


KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO
MGENI RASMI:
Mhe.GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
BUILDING A DIGITAL GOVERNMENT

# Kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) 2024



Aliyekuwa katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Donald Samweli, akiwaaga wajumbe baada ya kumaliza muda wake.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mha. Benedict Ndomba, akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi.




Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakiwa katika kikao cha Baraza.



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakiwa katika kikao cha Baraza.



Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji CPA. Salum Mussa pamoja na katibu wa Baraza la wafanyakazi wa e-GA Bi. Lina Kavishe wakifuatilia kikao cha Baraza la Wafanyakazi.



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Bw. Masuka Manyasi na Bw. Said Furu-tuni wakiwa katika kikao cha Baraza.

# KIKAO CHA WATUMISHI WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) KILICHOFANYIKA KUANZIA TAREHE 6-8 JANUARI 2024 KATIKA UKUMBI WA MAKUMBUSHO YA TAIFA JIJINI DAR ES SALAAM




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) akifungua kikao cha Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.




Afisa Uchunguzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Bi. Dorothea Mrema akitoa Mada wakati wa Kikao cha watumishi



Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakifuatilia Mada zilizokua zinatolewa wakati wa kikao wa Watumishi.



Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili Dkt. Garvin Kweka, wakati akitoa elimu ya afya ya akili kwa watumishi wa Mamlaka wakati wa kikao cha Watumishi wa Mamlaka.



Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji e-GA CPA. Salum Mussa akifurahia mada zilizokua zikitolewa wakati wa kikao cha watumishi.



Afisa anayeratibu Afua za VVU mahali pa kazi ngazi ya taifa, katika sekta ya umma kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Hafidh Ameir akitoa Mada wakati wa kikao cha watumishi.

# BONANZA LA MICHEZO

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakiongozwa na Mkurugenzi mkuu Mha. Benedict Ndomba wakishiriki katika michezo mbalimbali katika viwanja vya Gymkhana tarehe 8 Januari 2024 mara baada ya kushirki kikao cha watumishi














## SHUKRANI KWA UDHAMINI




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Damas Ndumbaro akikabidhi cheti cha Shukrani ya Udhamini wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini (TAGCO) kwa mwakilishi na Afisa Habari wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda




Waziri wa Habarii, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akikabidhi cheti cha Shukrani ya Udhamini wa Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Elimu kwa Umma kwa Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Edger Msamba

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE

Salum Mussa
Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

Hamis Ali
Meneja Ukaguzi wa Ndani

Rafael Rutaihiwa
Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai
Meneja wa Huduma kwa Wateja

## MHARIRI MKUU

Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI

Catherine Peter | Afisa Habari
Queenter Mawinda | Afisa Habari

## WAPIGA PICHA

Mussa Enock |Afisa Habari
Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA

Edger Msamba | Afisa TEHAMA